# UCHAMBUZI
# WA
# KITABU
# CHA
# **“WARAKA KWA WAEBRANIA”**

**Na Ap Shemeji Melayeki**

## **Siku ya 2**
## **SURA YA KWANZA**

**Waebrania 1**

***WAEBRANIA 1:1 Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,***

Kwenye KJV wanaandika Hebrews 1:1 ****God, who at sundry times and in divers manners spake in time past unto the fathers by the prophets,****

MUNGU ALIKUWA NA KAWAIDA YA KUJITAMBULISHA NA KUJIFUNUA KWA WAZEE WA KIEBRANIA KWA NAMNA MBALIMBALI KWA NJIA MANABII WALIOKUWEPO KABLA YA KRISTO, HII NI KUANZIA MWANZO MPAKA MALAKI.

KWENYE tafsiri ya AMPLIFIED ANASEMA ***_ALISEMA NAO IN MANY SEPARATE REVELATIONS, WHICH IS THE PORTION OF TRUTH. _****

__Yaani kwa mafunuo mbalimbali ambayo yalikuwa ni sehemu ya kweli…__ Ujumbe wa Mungu kwa wazee ulikuwa kwa sehemu nyingi (many portions), ambao ulisemwa kwa njia nyingi (divers manners)

**WAEBRANIA 1:2 mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.**

KUSEMA MWISHO WA SIKU HAKUWA ANAMAANISHA MWISHO WA DUNIA. HAPA MWANDISHI ANAMAANISHA ZAMA ZA MWISHO ZA MUNGU KUJIFUNUA KWA WATU. YAANI HAKUNA WAKATI MWINGINE WOWOTE MUNGU ATAKUJA KUJIFUNUA KWA MTU MWINGINE YOYOTE ISIPOKUWA KWA YESU KRISTO...

Jesus as a full revelation of God…. Or Revelation of God through Jesus Christ..

YOHANA MOJA ANAELEZEA VIZURI JUU YA UTENDAJI KAZI WA MUNGU NDANI YA YESU KRSITO.

***Yohana 1:1-5 Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima***

***ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.***

***Yohana 1:14 Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.***

***Yohana 1:18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.***

Neno aliyemfunua kwa Kigiriki (lugha mojawapo ya asili ya Biblia kabla haijatafsiriwa) ni *exēgeomai ambalo nomino yake ni exegesis* ambapo maana yake ni sawa na kuelezea, kufundishia, kuonyesha uhalisia (kuweka wazi). Ni sawa na kusema *exegesis* ya Mungu ni Yesu Kristo.

Kwa hiyo MSTARI WA 18 Yohana 1:18 Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.

Tungesema hivi,kama THEOLOGY IS THE STUDY OF GOD basi CHRISTOLOGY IS THEOLOGY. Kwamba Mungu amejifunua kwa njia ya Yesu Kristo ili tumjue… kumjua Mungu ni kwa njia ya Yesu Kristo..

KUMJUA MUNGU NI KWA NJIA YA YESU KRSITO… KWA HIYO TABIA HALISI YA MUNGU INAWEZA TU KUJULIKANA KWA KUMFAHAMU YESU KRISTO>

SABABU NI HII HAPA

WAEBRANIA 1:3 Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;

SABABU KUBWA NI KWAMBA MUNGU AMEWEKA MAMBO YOTE YANAMHUSU NDANI YA KRISTO, YAANI KRISTO NI BABA ALIYEFUNULIWA KATIKA MWILI. CHOCHOTE ALICHONACHO BABA NDICHO ALICHONACHO YESU. NDIYO MAANA ANAITWA MWANA YAANI *ALIYEFANANA NA BABA.*

***Yohana 10:30 Mimi na Baba tu umoja.***

***Yohana 15:24 Kama nisingalitenda kwao kazi asizozitenda mtu mwingine, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa wametuona mimi na Baba yangu, na kutuchukia.***

***Yohana 14:8-11 Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake. Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu; la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe.***

***Na kwa kisa hiki cha kuonyesha wazi wazi kwamba Yeye ni mwana wa Mungu Wayahudi walitaka kumpiga…***

WAEBRANIA 1:4 amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao.

MWANDISHI ANAONYESHA KUWA YESU NI BORA KULIKO MALAIKA, KWA SABABU MUNGU AMEMTUKUZA NA KUMPA JINA (NAFASI NA MAMLAKA) YAKE YOTE KAMA MWANAE.

WAEBRANIA 1:5 Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena, Mimi nitakuwa kwake baba, Na yeye atakuwa kwangu mwana?

HII NI KUYAPA HESHIMA MANENO YA MUNGU MWENYE JUU YA YESU AMBAYO YALIANDIKWA NA NABII DAUDI AKITABIRI HABAIRI ZA YESU KRISTO...

***Zaburi 2:7 Nitaihubiri amri; Bwana aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.***

***Matendo ya Mitume 13:33 ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya***

***pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.***

****YESU ALIZALIWAJE KAMA MWANA WA MUNGU?****

**LUKA (kwenye Matendo ya Mitume) AMETUPA TAFSIRI YA YESU ALIAMBIWA LINI KUHUSU KUZALIWA... KWENYE UFUFUO. Yesu anaitwa Mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu..**

***Matendo ya Mitume 13:33 ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.***

**PAULO ANAANDIKA HABARI HIYO AKIHUSISHA NA NAMNA MWAMINI ANAVYOZALIWA UPYA..**

**Wakolosai 1:3,13-15,18-19**

**[3]Twamshukuru Mungu, Baba yake Bwana wetu Yesu Kristo, siku zote tukiwaombea;**

**[13]Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;**

**[14]ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;**

**[15]naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, **mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.****

**[18]Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni **mzaliwa wa kwanza katika wafu,** _ili kwamba awe mtangulizi katika yote._**

**[19]Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae;**

Kwa lugha rahisi... MATUKIO YALIYOMPATA YESU YANAHESABIWA KAMA MATUKIO YALIYOMPATA MWAMINI..

KUTESWA pamoja naye,

Kufa na kufufuka pamoja naye...

Hii ni kwa sababu KRISTO YUKO NDANI YAKE..

Wagalatia 2:20

[20]Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.

Kila aliyezaliwa katika KRISTO, Kristo anakaa ndani yake... hivyo anaonekana aliypatwa na Yote yaliyompata Kristo na Ameshinda kama Kristo alivyoshinda...

Warumi 8:29

[29]Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

WAEBRANIA 1:6 Hata tena, amletapo **mzaliwa wa kwanza** ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.

YESU ALIKUWA MZALIWA WA KWANZA KUTOKA KWENYE MAUTI (KUFUFUKA) Yohana ameweka hilo wazi

***Ufunuo wa Yohana 1:5 tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake,***

***Wakolosai 1:18 Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.***

WAEBRANIA 1:7 Na kwa habari za malaika asema, Afanyaye malaika zake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa miali ya moto.

HII HABARI INAPATIKANA KWENYE ZABURI PIA.

***Zaburi 104:4 Huwafanya malaika zake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa moto wa miali.***

**KUWAFANYA KUWA PEPO na KUWAFANYA KUWA MOTO WA MIALI AU MIALI YA MTO MAANA YAKE Ni lugha ya picha tu kuwa ANAWATUMA ATAKAKO YEYE MUNGU. (MALAIKA = WATUMISHI) Malaika ni roho zinazotumwa...watumishi.**

**SASA MSTARI WA 8 HADI 12 ZINAZUNGUMZIA HABARI MOJA KWENYE ANGLE TOFAUTI… Kwa lengo hasa la kuonyesha ya kuwa Kristo ametukuzwa JUU YA MALAIKA.. ZOTE ZIKIWA ZIMENUKULIWA KWENYE VITABU MBALIMBALI VYA AGANO LA KALE**

WAEBRANIA 1:8 Lakini kwa habari za Mwana asema, Kiti chako cha enzi, Mungu,ni cha milele na milele; Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili.

WAEBRANIA 1:9 Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio.

HAYA MANENO YAMENUKULIWA KWENYE ZABURI PIA...

ANGALIA

***Zaburi 45:6-7 Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele, Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili. Umeipenda haki; Umeichukia dhuluma. Kwa hiyo MUNGU, Mungu wako, amekupaka mafuta, Mafuta ya furaha kuliko wenzako.*** **ZABURI HII YA DAUDI NI UNABII JUU YA NAFASI ALIYOPEWA YESU KWA SABABU YA KAZI YA MSALABA.... MWANA.**

WAEBRANIA 1:10 Na tena, Wewe, Bwana, hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi, Na mbingu ni kazi za mikono yako;

WAEBRANIA 1:11 Hizo zitaharibika, bali wewe unadumu; Nazo zote zitachakaa kama nguo,

WAEBRANIA 1:12 Na kama mavazi utazizinga, nazo zitabadilika; Lakini

wewe u yeye yule, Na miaka yako haitakoma.

NA HII PIA IMETOKA KWENYE

***Zaburi 102:25-27 Hapo mwanzo uliutia msingi wa nchi, Na mbingu ni kazi ya mikono yako. Hizi zitaharibika, bali Wewe utadumu Naam, hizi zitachakaa kama nguo; Na kama mavazi utazibadilisha, Nazo zitabadilika. Lakini Wewe U Yeye yule; Na miaka yako haitakoma*.**

WAEBRANIA 1:13 Je! Yuko malaika aliyemwambia wakati wo wote, Uketi mkono wangu wa kuume Hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako?

MWANDISHI ALIENDELEA KUCHAMBUA ZABURI...

***Zaburi 110:1 Neno la Bwana kwa Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwafanyapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako.***

***Luka 20:41-44 Akawaambia, Wasemaje watu kwamba Kristo ni Mwana wa Daudi? Maana, Daudi mwenyewe asema katika chuo cha Zaburi, Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwaweke adui zako Kuwa kiti cha kuwekea miguu yako. Basi Daudi amwita Bwana; amekuwaje mwana wake?***

HAPO YESU ALITAFSIRI MANENO YA DAUDI.

Daudi alipopata ufunuo juu ya Yesu Kristo hakumchukulia kama mwanawe bali BWANA WAKE. Petro pia alielezea hili siku ya ujio wa Roho Mtakatifu...

***Matendo ya Mitume 2:29-36 Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo. Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi; yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu. Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake. Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume.***

***Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako. Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.***

HAYA YOTE YANAONYESHA KUWA YESU KRISTO NI ZAIDI YA MALAIKA... NI BWANA, NI KRISTO, AMETUKUZWA KULIKO MALAIKA...

WAEBRANIA 1:14 Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?

**MWAndishi BAADA YA KUELEZEA NAFASI YA KRISTO, ANAPANUA ZAIDI KAZI NA NAFASI YA MALAIKA. KUWA HAO NI ROHO NA KAZI YAO KUBWA NI KUTUMIKA (WATUMISHI) WANATUMWA KUWAHUDUMIA WATAKATIFU. SASA HUDUMA YA MALAIKA NI HUDUMA PANA NA SIYO LENGO LA WARAKA HUU. UTAGUNDUA KWENYE SURA HII KUWA YESU AMEANZA KUINULIWA ILI APATE HESHIMA YAKE JUU YA MALAIKA. INAONEKANA WAEBRANIA WALIKUWA WANAAMINI SANA JUU YA MALAIKA KULIKO HATA YESU. KUSEMA HIVYO..**

**HAKUSHUSHA NAFASI YA MALAIKA LAKINI ALIMWEKA YESU KATIKA NAFASI STAHIKI...**

**MWANA VS MTUMISHI.**

**YESU KRISTO VS MALAIKA..**

**Kama ni hisabati tungesema __Hence Proved__**